

# Mapunda: Watendaji wanakwamisha miradi ya maji

- Mtanzania
- 15 Sep 2016
- Na GUSTAPHU HAULE -PWANI



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Erick Mapunda

LICHA ya Serikali kuweka msukumo na juhudi kubwa za kupunguza kero ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wake lakini wapo baadhi ya watendaji ambao wanachangia kukwamisha juhudi hizo.

Halmashauri ya Wilaya ya Mafia iliyopo mkoani Pwani ni miongoni mwa Halmashauri ambazo zilibahatika kupata miradi mikubwa ya maji lakini baadhi ya watendaji wamekwamisha miradi hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Erick Mapunda, anasema amebaini kuwapo kwa miradi mikubwa miwili ya maji iliyoanza kutekelezwa tangu mwaka wa fedha 2012/13.

Mapunda anasema miradi hiyo ilifadhiliwa na benki ya dunia kupitia Serikali Kuu chini ya mpango wa miradi ya maji na usafi wa mazingira (National Water Sector Development Program (NWSDP).

Anasema katika mpango huo, Halmashauri ya Wilaya ya Mafia ilipata miradi 10 ambayo inatekelezwa katika vijiji 10 vilivyopo katika Kata mbalimbali.

Anasema vijiji hivyo ni pamoja na Kangana na Bweni (Kata ya Kanga), Jimbo na Kirongwe (Kata ya Kirongwe), Chunguruma (Kata ya Ndagoni), Kungwi na Kibada (Kata ya Baleni), Mlongo (Kata ya Miburani), Chole, Juani na Jibondo (Kata ya Jibondo).

Anasema ili kutekeleza na kukamilisha miradi hiyo Serikali za Vijiji vilivyonufaika vilipaswa kuchangia fedha kiasi cha asilimia 2.5 ya gharama nzima ya mradi ambapo matumizi yake yanaratibiwa na Serikali ya Kijiji.

Mapunda anasema mradi wa Kijiji cha Kanga uliogharimu zaidi ya Sh milioni 360 ulikamilika Desemba 2014 na kukabidhiwa rasmi kwa Serikali ya Kijiji Januari 26 mwaka jana ukiwa unafanya kazi kikamilifu.

Anasema tangu kukabidhiwa kwa mradi huo, uendeshaji wake umekuwa na mapungufu makubwa na hivyo kushindwa kufanya kazi ipasavyo jambo ambalo limesababisha wananchi waliokuwa wakitegemea mradi huo kukosa maji.

Mkurugenzi huyo anasema mapungufu yaliyopo katika mradi huo yamebainika Agosti 14 mwaka huu baada ya kufanya ziara na watendaji wake iliyokuwa na lengo na kuona maendeleo ya miradi ya maji vijijini.

Anasema mapungufu hayo ya mradi huo kutelekezwa na kutohudumiwa maeneo yake ya utekelezaji, mabomba kupasuka kutokana na mradi kutofanya kazi, mapato yatokanayo na mauzo ya maji kutopatikana pamoja na jumuiya ya watumiaji maji kutosimamia kikamilifu.

Anasema mapungufu mengine ni Serikali ya Kijiji kutosimamia vyema jumuiya ya watumiaji maji pamoja na kushindwa kufanya vikao vya uendeshaji wa mradi huo.

“Serikali imetoa fedha nyingi katika ujenzi wa mradi huu lakini bado watendaji wa ngazi ya kijiji wameshindwa kusimamia jambo ambalo linasababisha wananchi kutumia maji ya visima vifupi ambayo si salama,” anasema Mapunda.

Anasema kutokana na mapungufu yaliyopo katika mradi huo tayari amechukua hatua kwa kumsimamisha kazi kaimu afisa mtendaji wa Kijiji cha Kanga ambapo nafasi hiyo imeshikiliwa kwa muda na Sadiki Sinde.

Anasema hatua nyingine iliyochukuliwa ni kuvunja kwa jumuiya ya watumiaji maji ya Kijiji cha Kanga na kuundwa upya na kufanyika kwa ukaguzi maalumu kwa viongozi na watendaji wa kijiji juu ya mapato na matumizi ya fedha zilizotokana na makusanyo ya michango ya maji.

Salma Rashid (39) Mkazi wa Kijiji cha Kanga, anasema kabla ya mradi huo walikuwa wakiteka maji katika visima vifupi vilivyokuwepo mbali na makazi yao japo si safi na salama.

“Wakati mwingine nilikuwa nikitumia kutwa nzima kutafuta huduma ya maji na matokeo yake shughuli zangu za kujitafutia kipato zilikuwa zikisimama,” anasema Salma.

Anasema baada ya mradi huo kukamilika na kukabidhiwa katika serikali ya kijiji walipata maji kwa muda wa miezi nane na baadae ulikufa kwakuwa ufuatiliaji wake haukuwa mzuri.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kanga, Makungu Khatibu, anasema mradi huo ulikufa kutokana na jumuiya ya watumiaji maji kukosa ushirikiano wa kutatua kero zinazojitokeza.

Mkurugenzi huyo anasema pia katika Kijiji cha Chabweni kumegundulika kuwa na vyanzo vingi vya maji yenye asili ya chumvi isipokuwa katika Kitongoji cha Ukanda.

Anasema kwasasa Kitongoji cha Ukandi upo mradi wa Sh milioni 461 lakini ulichelewa kutekelezwa kutokana na wananchi wake kuzuia usambazaji wake katika maeneo mengine yaliyopo nje na kitongoji chao.

Mapunda anasema baada ya majadiliano na uelimishaji uliofanyika katika mkutano mkuu wa kitongoji cha ukanda, changamoto hiyo imemalizika na kwamba mradi huo unaendelea vyema huku akiwahimiza wananchi hao kuchangia asilimia 2.5.

Mkurugenzi huyo anawataka wananchi waliopo jirani na miundombinu ya usambazaji maji kuitunza kikamilifu na ikiwezekana watunge sheria ndogondogo zitakazosaidia kuwabana watu watakaoharibu.